# UJUZI WA MAWASILIANO

Endapo utajikuta ukiwa peke yako jangwani, ni wazo gani litakalokujia kwanza? Naamini halitakuja kwanza wazo la kufikiria wanyama pori ama utajiri wako, ama hata kiwango chako cha elimu. Na bila shaka, wazo litakalokujia kwanza ni kuhusu jinsi gani utawapata watu wa kushirikiana nao. Hili ni wazo lililojengeka ndani ya kila mwanadamu. Tuliumbwa katika hali ya kuhitaji ushirikiano baina ya mtu na watu wengine. Ili kuondoa upweke huu wa mtu kukosa usaidizi; Mungu alihakikisha kwamba kila mtu anakuwa na kipaji chake kisichokuwa kwa mwingine ili kwa njia hiyo tuweze kuwaendea wengine kwa kusaidiana. Kama unataka kufahamu jinsi ambavyo familia za wanadamu zinavyotegemeana; na jinsi tusivyoweza pasipo watu wengine; basi hebu tuviangalie viungo vya mwili wa binadamu. Hili litatupa ufahamu wa wazi na ulio thabiti.

Katika namna hii ya muungano wa kikazi; naam, katika kushikamana na kusaidiana baina ya mtu na mtu kwa kadiri iwezekanavyo, tunapaswa kuwa na mikutano endelevu. Lakini je! ni kwa namna gani tunapaswa kufanya hivyo?

## MAWASILIANO

Naam; ni kwa njia ya mawasiliano. Lakini je! mawasiliano yanasaidia nini? Ili tulifahamu jambo hili vizuri, tunahitaji kwanza kufahamu kwamba mawasiliano ni nini hasa. Mawasiliano ni shughuli ama mchakato wa kuelezea mawazo au hisia, ama kuwapa/kuwapasha watu habari. Mazungumzo ndiyo njia ya kwanza ya kuwasiliana baina ya watu.

Kwa njia ya mawasiliano, mtu huwashirikisha wengine mawazo yake ya kutaka kufanya jambo, hisia zake na matamanio yake; naam, kadhalika hata kero na huzuni ama sikitiko lake. Sasa basi; ili jambo hili lifanyike kikamilifu, tunahitaji kujifahamu kwanza. Sisi si kama *{si sawa na}* Mungu. Na hivyo basi; kuna vitu vilivyo nje ya ufahamu wetu kujua, na pia viko nje ya uwezo wetu kutenda. Muumba wetu anatuambia kwamba; *"hakuna mtu ajuaye mawazo ya mtu mwingine isipokuwa roho yake tu"*, ***soma 1 Wakorintho 2:11.*** Hapo *{katika moyo wa mtu}* ndipo mahali ambapo msukumo wa mawasiliano unapotokea, na ndiyo maana hatuwezi kuwasiliana pasipo hili. Kwa hivyo mtu anapoamua kukaa kimya bila kuwashirikisha wengine yaliyo ndani ya moyo wake, basi mtu huyo anakuwa/anaonekana mgeni na haiwezekani kumsaidia kwa namna yo yote ile. Watu watabakia kumdhania tu, na katika kutaka kumsaidia, watazidi kumshambulia tu zaidi ya kumsaidia.

Kwa vile kila mmoja anahitaji maisha yaliyo makamilifu na mepesi, basi tunahitaji habari kutoka na kwenda kwa wengine ili kulifanikisha hilo. Tunahitaji kupata vipaji kutoka kwa

wengine, vile vile kama ambavyo wao pia wanavyohitaji vipaji vyetu wasivyokuwanavyo. Na hili linahitaji uwazi kutoka pande zote. Unahitaji msaada? Wasilisha matatizo yako kwa uwazi kwa wengine ili wayafahamu, na wakiisha kuyafahamu, watakupa suluhisho la matatizo yako. Unahisi kutaka kuwasaidia wengine? Usifanye kwa kudhania tu; na badala yake, ngojea kwanza wakupe habari kamili kuhusu matatizo yao.

## MAWASILIANO, ADUI MKUBWA

Mungu ametuambia wazi kwamba, haiwezekani kuyafahamu mawazo ya mtu mwingine endapo mtu huyo hajakwambia yeye mwenyewe. Jambo baya ambalo kizazi cha leo kinalitumia katika kuhusiana baina yao ni madhanio *{kwa kuwazia/kufikiria};* na hili linafanyika kwa kuwa mwingine hataki kuwasiliana. Kudhania ni kutengeneza picha ama wazo akilini mwako kuhusu namna kitu kinavyoweza kuwa ama kilivyo. Ni kuamini kitu ambacho mtu anakitengeneza akilini mwake na ambacho si ukweli ama uhalisia wenyewe. Jambo hili ni adui mkubwa wa mawasiliano na sababu *{chanzo}* ya vurugu za kila namna katika jamii yote ulimwenguni leo. Hili linapeleekea kile ambacho Mungu anakiita kama **"kuwahukumu wengine",** na ni jambo alilokataza ***{soma Mathayo 7:1}.*** Endapo mtu atadhania kitu fulani kuhusu mtu mwingine aliye mgonjwa na kutumia dhana hiyo katika kumtibu mtu huyo, basi matokeo yatakuwa hasi na kutatokea athari za matibabu mabaya. Migogoro yote hii tuionayo duniani leo, chimbuko lake hutokana na huku kudhania.

Je! unafahamu chanzo *{chimbuko}* chake? ***"…nanyi mtakuwa kama Mungu…", soma Mwanzo 3:5.*** Mungu yukoje? ***"…maana wewe*** *{Mungu}* ***peke yako ndiwe uijuaye mioyo ya wanadamu wote" 1 Wafalme 8:39.*** Naam; wanadamu wanajidhania wenyewe kuwa wako kama Mungu na hivyo kwamba wanafahamu kila kitu. Wanajaribu kusoma mioyo ya wenzao na kujipatia majibu kutokana na ujinga wa mioyo yao ***{soma Yeremia 17:9}.***

Basi eleweni na fahamuni kwamba; hii ni njia *{mbinu}* mbadala ya Shetani yenye lengo la kuleta migawanyiko na mapambano baina ya wanadamu wenyewe kwa kusudi la kuwaharibu na kuwaua wote. Naam; madhanio ni zao *{tunda}* la udanganyifu wa Edeni.

## TUFANYE NINI BASI?

*"Usifanye mambo kulingana na mawazo yako mwenyewe; katika kila jambo rejea kwa Mungu, naye atayanyoosha mapito yako",* ***soma Mithali 3:5.*** Mungu yupo hapa akisema; *"usidhanie; uliza na utaambiwa. Tafuta maarifa kutoka kwa watu wengine na utayapata".*

Ustaarabu wa leo umejengwa juu ya madhanio; na tunaamini kila mmoja anashuhudia matokeo yake. Taarifa za migogoro zimejaa kila kona ya dunia. Hakuna nchi hata moja

isiyoshuhudia matokeo ya watu kutumia dhana zao badala ya kutumia ukweli wa mawasiliano. Mwanzilishi wa maisha alilianzisha kanisa lake ili kuwaonesha wanadamu wote kile alichokuwa amekikusudia moyoni mwake pindi alipotuumba. Naam; anasema; ***"…na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote; ili sasa kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane…" Waefeso 3:9-10.***

Kwa hivyo; katika ulimwengu uliogawanyika kwa kila aina ya migogoro; Mungu anawachagua watu *{ambao ndio Kanisa lake}* na kuwafanya watoke katika huu udanganyifu wa Edeni, ili wapate kuuonesha ulimwengu mfano mzuri wa namna ya kuwasiliana na kuwa na familia moja ya wanadamu iliyo ya kweli ambayo kila mmoja atakuwa kiungo kwa mwingine. Ni maagizo *{mwongozo}* gani ambayo Mungu amelipatia Kanisa lake na ambayo anayakusudia kwa wanadamu wote kwamba wapate kuishi kwayo?

## KUJIKANA NAFSI

Kwa kuwa kile tunachofahamu na kudhania kuhusu nafsi zetu wenyewe ni ule udanganyifu *{uongo}* wa Edeni; basi tunapaswa kuanza kwa kujikana nafsi zetu kwanza ***{soma Mathayo 16:24}.*** Kufanya hivyo kutazipatia akili *{nia/mioyo}* zetu nafasi iliyo wazi na isiyo na ufahamu wo wote ule. Na kisha baada ya hapo; tukiri *{tukubali}* kwamba Biblia ni mwongozo *{dira}* wa Mungu kwa wanadamu unaohusu namna ya kuishi.

Mara tutakapochukua hatua hiyo; basi mawasiliano yatakuwa mepesi sana, maana hakuna atakayeipigania wala kuilinda nafsi yake, na badala yake, sote tutajitahidi *{tutapigania}* kufanya mambo yaliyo mema na ya kweli. Hatutazungumza tena kwa namna ya mtu kutaka kujionesha kuwa yeye ni bora ama mkubwa zaidi ya wengine; maana tutafahamu kwamba sisi ni mavumbi tu, na ni kama majani *{soma Mwanzo 18:27; Zaburi 103:14-15}.*

Kwa hivyo basi; itakuwa rahisi kuungana tukiwa na nia *{akili}* hii moja ya kujitahidi kuwa kama Mungu, na wala si kuwa kama mmoja wetu. Hatutakuwa na cho chote cha kuficha kuhusu nafsi zetu, na hivyo tutakuwa wa wazi kwa wengine ili kupata habari za hakika kwa wengine.

Ikiwa kila mmoja atajitahidi kwa dhati kupigania kuwa kama Mungu na kuwa na nia ya kutaka kusikiliza kile asemacho *{kuhusu kila jambo}* katika mwongozo wake *{yaani, Biblia},* tutasema nini basi? Tutatofautiana kwa lipi? Tutajaribu kuficha kitu gani? Mungu ni mmoja; kadhalika na njia *{namna}* yake ya maisha pia ni moja. Endapo tutamgeukia yeye *{kila mtu mmoja mmoja},* tutachukua nia yake moja, na kuwa na mawasiliano ambayo yatatufanya kuwa wenye *"kunena mamoja; wala tusiwe na mafarakano, bali tuwe wenye nia moja na shauri moja",* **soma 1 Wakorintho 1:10.**

Wapendwa; tunayo mengi ya kuzungumzia kuhusiana na jambo hili, lakini nafasi haitoshi. Kwa sababu hiyo basi; tunakushauri kuagiza majarida na vitabu vyetu vingine ili ujifunze mengi zaidi. Huduma yetu inatolewa bure kabisa kwako pasipo malipo yo yote utakayotozwa; maana Kristo Yesu aliyetutuma ametuagiza akisema; ***"…mmepata bure, toeni bure. Msichukue dhahabu, wala fedha, wala mapesa mishipini*** *{ama mifukoni}* ***mwenu" Mathayo 10:8-9.*** Kwa hivyo wewe agiza tu majarida ama vitabu vile utakavyopenda kujifunza, nasi tutakutumia huko uliko wewe.

Tunayo majarida yenye mada mbali mbali kama vile; THAMANI YA UKRISTO, KUOKOLEWA KWA NEEMA, KANISA LA SIKU ZA MWISHO, JE, WEWE NI MKRISTO?, ROHO YA SABATO ZA BWANA, SHETANI NI NANI?, SHERIA ZA KIAFYA, HUYU NI SHETANI, MITI MIWILI n.k.

Pia tunavyo vitabu vyenye mada mbali mbali kama vile; UFALME WA MBINGUNI, SIKUKUU ZA MUNGU, KIFO NA KIYAMA, AMRI KUMI, DINI ZA MITINDO, BIBLIA NA AFYA ZETU, n.k. Hivi vyote viko tayari kabisa kwa ajili yako; nasi pia tuko tayari kabisa kukuhudumia.

**Basi wasiliana nasi kwa anuani zifuatazo:-**


**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Nambari za simu: +255 753 359 179, +255 688 359 179 na +255 655 659 179.**

**Barua pepe: Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg**

**NA**

**KANISA LA MUNGU – KENYA**

**Barua pepe: endcog@gmail.com**


***Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Utukufu una yeye tangu milele, sasa na hata milele; Amina.***